HOTUBA YA MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI (MB.), WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS- MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA KATIKA UFUNGUZI WA MDAHALO WA WADAU KUHUSU KUJENGA NA KUKUZA MAADILI, HAKI ZA BINADAMU, UWAJIBIKAJI, UTAWALA BORA NA MAPAMABANO DHIDI YA RUSHWA KATIKA UKUMBI WA MAKUMBUSHO YA TAIFA-DAR ES SALAAM

30 NOVEMBA, 2016.

Profesa Mussa Assad, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na Kaimu Mwenyekiti wa Kamati Kuu ya Maandalizi;

Mhe. Bahame T. Nyanduga, Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora;

Dkt. Laurent Shirima, Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Ununuzi wa Umma;

Bwana Mathew M. Kirama, Mkurugenzi wa Idara ya Ukuzaji Maadili, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;

Bibi, Rose Kilango Elipenda, Kaimu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma;

Bibi. Stella Mpanju, Mkuu wa Sehemu ya Elimu kwa Umma, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU);

Bibi. Christina Maganga, Mratibu wa Utawala Bora, Ofisi ya Rais - IKULU

Watoa Mada;

Viongozi wa Serikali na Wawakilishi;

Wawakilishi wa Viongozi wa Kidini;

Wawakilishi wa Vyama vya Siasa;

Wawakilishi wa Vyama vya Wafanyabiashara;

Wawakilishi wa Asasi za Kiraia;

Wahariri wa Vyombo vya Habari;

Wawakilishi wa Kutoka Elimu za Juu;

Watumishi wa Umma;

Wageni Waalikwa;

Waandishi wa Habari; na

Mabibi na Mabwana.

Habari za Asubuhi.

Awali ya yote ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii kushiriki nanyi katika ufunguzi wa mdahalo huu wa wadau unaohusu masuala ya Maadili, Haki za Binadamu, Uwajibikaji, Utawala Bora na Mapambano Dhidi ya Rushwa.

Nafahamu kwamba Mdahalo ni wapili kufanyika kitaifa, katika kuadhimisha siku ya Maadili na Haki za Binadamu Disemba 10, 2016. Nitumie nafasi hii kukushukuru wewe binafsi Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Maadhimisho pamoja na Wakuu wote wa Taasisi zinazoratibu Kampeni hii kwa heshima kubwa mliyonipa, kunialika kwa nafasi ya Mgeni Rasmi.

Pia ninapenda kuwapongeza wadau wote ambao mmeona ni vyema na busara kutenga muda wenu kwa ajili ya kushiriki katika mdahalo huu.

Ni wahakikishie kuwa uwepo wenu hapa ni muhimu sana sio tu katika kufanikisha malengo ya mdahalo huu bali pia katika kujenga utamaduni wenye maadili mema kwa kizazi hiki na vizazi vijavyo. Ahsanteni Sana.

Ndugu Washiriki;

Kama nilivyo kwisha kusema huu ni mdahalo wapili ambao unafanyika baada ya Mdahalo wa Kwanza wa Tarehe 22 Novemba 2016 ambao ulihuisha wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari. Midahalo hii ni muhimu sana na imekuja wakati muafaka kwa kuwa Taifa letu lipo katika changamoto kubwa ya kuhakikisha nchi yetu inajengwa na kukuzwa katika maadili.

Ndugu washiriki;

Maadili ni hatua muhimu sana ambayo humtambulisha mtu ndani ya jamii yake na katika hali ya kawaida Maadili hujitokeza katika matendo kwa vile ndicho kilelezo sahihi cha kupima Maadili ya jamii. Kauli mbiu yetu ni, "Kujenga na Kukuza Maadili, Haki za Binadamu, Uwajibikaji, Utawala Bora na Mapambano Dhidi ya Rushwa". Lengo la kuwa na kauli mbiu hii ni kuunga mkono jitihada za Serikali ya Awamu ya tano inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli za kupinga vitendo vya Rushwa, Uzembe, Ufisadi na Matumizi Mabaya ya Fedha za Umma na Ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu.

Ndugu Washiriki;

Maadili ni suala linalopewa kipaumbele na Serikali ya Awamu ya Tano. Mtakubaliana na mimi kuwa Mhe. Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli katika mikutano yake yote amekuwa akiwasihi sio tu watumishi wa umma bali pia wananchi kwa ujumla kurudia Maadili yetu.

Katika kipindi chake cha mwaka mmoja wa uongozi amekuwa akionesha kwa vitendo jinsi gani anachukizwa na ukiukwaji wa maadili, haki za binadamu, ufisadi hata kukemea wazi wazi rushwa na harufu za rushwa katika Serikali yake mwenyewe.

Ndugu Washiriki;

Mimi nikiwa Waziri wa Nchi, mwenye dhamana ya kusimamia Maadili katika Utumishi wa Umma, sitaacha kutoa kipaumbele katika kushirikisha jamii nzima kwa ujumla kupambana na vitendo vya ukiukwaji wa Maadili, Haki za Binadamu, Uwajibikaji, Utawala Bora na Mapambano Dhidi ya Rushwa.

Ndugu Washiriki;

Pamoja na majukumu mengi niliyopewa kuyatekeleza kwa nafasi hii, bado niseme kwamba kutokana na umuhimu wa Mdahalo huu kwa jamii au taifa letu katika kutimiza dhana ya utawala bora ambapo uwazi na uwajibikaji ni nguzo muhimu ya Utawala Bora, suala la ushiriki na ushirikishwaji wa wadau mbalimbali wa masuala ya Maadili ni lakupewa kipaumbele hivyo niwaombe ndugu zangu kila mmoja kwa nafasi yake, tusirudi nyuma tufanye sehemu yetu.

Ndugu Washiriki;

Ili kufanya suala la maadili lisiwe la kipindi cha kampeni tu, sisi wadau wa masuala haya tunatakiwa kuelewa kuwa suala la Kujenga, Kukuza na Kusimamia Maadili siyo jukumu la Mheshimiwa Rais wetu Dkt; John P. Magufuli peke yake, au

Taasisi za usimamizi peke yao au Viongozi wa Dini, wala siyo jukumu la vyama vya siasa au vyombo vya dola nchini, bali ni jukumu la jamii nzima. Hivyo, nitoe rai kwa jamii nzima kuwa sote tushirikiane kwa pamoja katika ngazi zote na hasa sisi tuliohudhuria leo tuwe mabalozi wa kwanza kufikisha ujumbe vizuri kwa jamii.

Ndugu Washiriki;

Nimearifiwa kuwa katika mdahalo huu kutakuwepo na uwasilishwaji wa mada mbalimbali ambazo zimeandaliwa ili kutoa muelekeo wa mjadala mpana wa masuala ya Maadili, Haki za Binadamu, Uwajibikaji, Utawala Bora na Mapambano Dhidi ya Rushwa, ni matarajio yangu kuwa wote tutapata fursa ya kutoa michango itakayosaidia kuondokana na changamoto nyingi za kimaadili zinazotukabili hivi sasa.

Ndugu Washiriki;

Sio siri kuwa kadiri siku zinavyoenda suala la maadili ni changamoto sio tu kwa Tanzania bali hata dunia kwa ujumla. Vitendo vya Rushwa, Ufisadi na Ukiukwaji wa Haki za Binadamu vimeendelea kuwa ni tatizo la dunia nzima. Kwa mfano tatizo la Mauaji ya Kutisha ya ndugu zetu wenye ulemavu wa ngozi kwa kiasi kikubwa linachangiwa na ukiukwaji wa maadili. Je vyombo

vya dola peke yake vinaweza kumaliza matatizo haya? Ni ukweli usiopingika kuwa peke yake matatizo haya hayawezi kumalizika. Tunahitaji jamii nzima ipinge, ikemee na kutokomeza vitendo vyote vya ufisadi, rushwa, ukiukwaji wa maadili na haki za binadamu ili kuliletea taifa letu maendeleo endelevu. Hii haimaanishi kuwa Serikali ya Awamu ya Tano haitatekeza majukumu yake ya msingi katika kuhikiza uzingatiaji wa maadili, la hasha, tutaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kinidhamu na kisheria ili kupunguza kama sio kumaliza matatizo haya.

Ndugu Washiriki;

Serikali katika kipindi hiki cha uwepo wa mmomonyoko wa maadili unaotokana na utandawazi na mambo mengine, imeendelea kutoa maelekezo mbalimbali yanayolenga katika kurejesha nidhamu na maadili kwa watumishi wa umma na jamii kwa ujumla kwa sababu watumishi wa umma hawawezi kukiuka taratibu za utumishi bila kushirikiana na mwanajamii katika aidha kutotenda haki au kufanya ubadhirifu wa mali za umma.

Ndugu Washiriki;

Pamoja na Serikali kuweka utaratibu mzuri wa namna ya kushughulikia matatizo ya utovu wa nidhamu, rushwa au ubadhirifu wa mali za umma bado tumeendelea kushuhudia

changamoto mbalimbali na nisisitize tu kwamba serikali inaona kuna umuhimu mkubwa na haja yakuendelea kushirikisha au kuhimiza makundi yote kwa pamoja kuhakikisha tunaondoa tofauti na vikwazo ili kutimiza adhima iliyokusudiwa ya kumpa mwanafunzi elimu na stadi bora, kwa kujenga misingi ya maadili inayokubalika kitaifa na uwepo kwa ushirikiano wa pamoja.

Ndugu Washiriki;

Baada ya kusema hayo machache niiombe tu waratibu wa kampeni hii ihakikishe inaandaa taarifa kamili na sahihi ya tathmini ya kampeni hii ya mwezi ili yale yatakayokuwa yameibuliwa kupitia aidha vyombo vya habari, matembezi ya hiari au Midahalo ya namna hii na yanaigusa Serikali moja kwa moja katika mabadiliko ya Sera, Sheria, Kanuni au taratibu tuweze kuyafanyia kazi kwa kuchukua hatua stahiki kwa wakati.

Ndugu Washiriki;

Napenda kusema kuwa kwa heshima na taadhima, sasa natamka kuwa Mdahalo huu sasa nimeufungua rasmi.

AHSANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA.